**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Namba za simu
Mkuu wa shule 0764017014
Makamu mkuu wa shule 0679154729

Shule ya Sekondari Bunazi,
S.l.p 79,
**Kyaka.**
**Tarehe……………**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi
…………………………………………
S.L.P……………………………………..
…………………………………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI BUNAZI, HALMASHAURI YA WILAYA MISSENYI MKOA KAGERA MWAKA 2023.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2023 tahasusi ya……………Shule ya Sekondari **Bunazi** ipo umbali wa Kilometa **0.5** Kusinimwa mji wa **Bunazi** Usafiri wa basi kutoka Mjini Bukoba unapatikana katika kituo cha mabasi Bukoba nauli ni shilingi 3,000/= (Elfu tatu) tu. Mwisho wakuripoti shuleni ni saa 12:00 jioni

Anatakiwa kuripoti shuleni tayari kwa kuanza muhula wa kwanza tangu tarehe 14/08/2023 mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 31/08/2023 Akichelewa kuripoti shuleni zaidi ya wiki mbili bila sababu maalumu baada ya shule kufunguliwa, anaweza kupoteza nafasi yake. Siku za kuripori wanafunzi ni **Jumatatu mpaka Ijumaa kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 12:30 jioni.**

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1. **SARE YA SHULE**

i) Mwanafunzi anatakiwa kuja Sketi mbili (2) rangi ya dark blue, mshono lindaboksi (lindaboksi kubwa moja mbele na nyuma) na Mashati meupe mawiliyenye mikono mirefu yasiyobana.

***Angalizo***: yasiwe ya mtumba.

(ii) Wanafunzi wa kiislamu, nusu kanzu nyeupe mbili za kitambaa cha tetroni nzito na hijabu (juba) nyeupe mbili ndefu zinazofunika kifua zisizo na urembo wa aina yeyote na zisizobana. zisizo na Vyote vikiwa na rangi nyeupe na mikono mirefu (tetron) yasiwe ya mitumba. Urefu wa sketi uwe robo tatu ($^{3}/_{4}$) ya urefu wa kutoka kwenye kiuno mpaka usawa wa nyayo.

Mfano; Kama urefu wa kutoka kwenye kichwa mpaka kwenye kiuno ni sm 100. Nusu kanzu najuba viwe na urefu wa sm 75.

iii) Sare ya michezo kwa shule hii ni Track Suits moja za rangi ya blue bahari na T-shirt moja rangi nyekundu pamoja na raba jozi moja.

iv) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

v) Soksi jozi mbili nyeupe za shule.

vi) Sweta moja ya rangi ya kijani.

vii) Nguo za kushindia (shamba dress) ni sketi mbili rangi ya kijani (kitambaa cha sukari malinda 16) na T-shirt nyekundu

viii) Tai moja ya rangi ya dark blue.

***NB:*** *Ni muhimu mwanafunzi kuja na mwavuli na buti kwani maeneo haya ni ya mvua nyingi. Mwanafunzi pia aje na tochi au taa ndogo za solar kwa ajili ya kumsaidia usiku pidi tu umeme unapokatika.*

**2. 2. MICHANGO YA SHULE**

2.2. a) **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

Ili kuhakikisha kwamba shule inaendelea kutoa huduma iliyo bora tunakuomba mzazi/mlezi kuchangia michango ifuatayo:-

**NB:** Michango yote ilipwe benki ya NMB akaunti namba ya shule 3261100008

**Bunazi secondary school reccurent.**Hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye pay-in-slip.

Michango inayotakiwa kulipwa kwa kila mzazi/mlezi ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

| Na | MICHANGO | KIASI (TSHS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= | Lipia benki |
| 2 | Nembo | 5,000/= | Lipia benki |
| 3 | Tahadhari | 5,000/= | Lipia benki |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= | Lipia benki |
| | **JUMLA** | **80,000/=** | |

***MUHIMU: I Kila mwanafuzi aripoti shuleni akiwa na bima ya afya.***

**b) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i) Ream (A4) ya karatasi 2 kwa mwaka.

ii) Madaftari makubwa counter book (quire 4) kumi (10).

iii) Oxford Dictionary- Advance learners.

iv) Kamusi ya Kiswahili.

v) Karamu za wino, za risasi, rula na raba.

vi) Mashuka mawili (2) rangi ya pinki, blanketi moja (1), mto pamoja naforonya moja (1) rangi ya pinki, chandarua kimoja (1) rangi ya blue, godolo futi 2½ (super banco).

vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuri, kijiko na kikombe).
viii) Taulo, kitenge kimoja cha kujifunga wakati wa kwenda kuoga.
ix) Galeni/chombo chochote chenye uwezo wa kutunzia maji ya kunywa (lita 5 au zaidi).
x) Mafuta ya kujipaka, dawa ya meno, ndala, toilet paper (mikunjo 6) na dawa ya viatu.
xi) Viatu vya wazi vya kuvaa baada ya masomo.
xii) Ndoo mbili zenye mifuniko.
xiii) Mfagio wa chelewa wenye mpini mmoja, Hard bloom moja (brush ngumu yenye mpini), Soft bloom1 (brush nyepesi mfagio wa ndani), squeezer (mfagio wa kukaushia maji, jembe lenye mpini, reki 1, fyekeo 1 na kotama 1. Ili kuepusha usumbufu vifaa hivi unaweza kuvipata kwenye maduka yaliyopo karibu na shule.
xiv) Picha (passport size) nne (4), utapata huduma hii shuleni.

### C) MAHITAJI MENGINE YA KITAALUMA.

Mwanafunzi anayeripoti ahakikishe analeta viambatanisho vya kitaaluma vifuatavyokwa ajili ya matumizi ya ofisi:
i.Nakala ya cheti halisi cha kuzaliwa (Birth certificate).
ii.Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne (Leaving certificate).
iii.Nakala ya hati ya matokeo ya kidato cha nne (Results slip).

***NB:*** Mzazi/Mlezi anashauriwa kumnunulia mwanafunzi japo kitabu kimoja kimoja kwa masomo atakayosoma hapa shuleni kulingana na tahasusi aliyopangiwa.

### D) MAHITAJI YA VITABU VINAVYOTAKIWA.

Mzazi/mlezi kumbuka kwamba, ili mwanafunzi aweze kutimiza malengo yake ya kitaaluma, anapaswa pia awe anasoma vitabu. Unaombwa na**bodi ya shule** kumnunulia mwanao angalau **kitabu kimoja** kwa kila somo kulingana na masomo anayosoma (VITAKAGULIWA SIKU YA KURIPOTI SHULENI).

| S/N | SOMO | AINA YA KITABU |
|---|---|---|
| 01 | HISTORY | -Essential in Advanced level History –paper 1 by SALEHE YASIN<br>-Essential in Advanced level History-paper 2 by SALEHE YASIN<br>-CK. Shibitali (2015, 2016, 2017 edition) Contemporary world Events.<br>-D.E. Butendeli (2016) Major trands in world history from Medieval era to Present advanced level Comprehensive Note. History paper two.<br>-Oxford Advanced Learners history form 5. |
| 02 | KISWAHILI | -Fonolojia ya Kiswahili sanifu(FOKISA) sekondari na vyuo By MASSAMBA DPB na WENZAKE<br>-Fasihi ya Kiswahili, chuo kikuu Huria cha Tanzania By MULOKOZI, MM 1996<br>-Nadharia ya lugha Kiswahili moja kidato cha tano na sita – Nyambali Nyangwine<br>-Nadharia ya lugha Kiswahili mbili kidato cha tano na sita fasihi kwa ujumla<br>-Tahakiki ya vitabu teule kidato cha tano na sita. |
| 03 | ENGLISH LANGUAGE | 1. The Real English Text Book For Advanced Level Form 5 & 6 By KADEGHE MICHAEL, 2010<br>2. Advanced English language, Form 5 & 6 By DSM OXFORD UNIVERSITY PRESS, 2012 |

| | | |
|---|---|---|
| | | 3. Oxford Advanced Learner's Dictionary |
| 04 | FRENCH LANGUAGE | ANY ENGLISH- FRENCH DICTIONARY<br>Grammaire du francais( any)<br>Les livres pour conjugaisons |
| 04 | GENERAL STUDIES | 1. Understanding Advanced level General studies By JAMES BIGIRAMUNGU & SM. DEOGRATIAS 2012<br>4. Comprehensive book for advanced level secondary schools – Mwajabu B. Mruma<br>5. General Studies – Nyambali Nyangwine<br>6. General Studies Alive – Zisti Kamili |

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebiswa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:

### 03.01: Sheria na kanuni za shule.

Sheria za shule zimewekwa ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya taifa, shule na mwanafunzi mwenyewe. Hivyo mzazi/mlezi na mwanafunzi ambaye ndiye mlengwa haswa, anapaswa kuzisoma kwa makini, kuzitafsiri, kuzielewa na kuzitii wakati wote ili malengo yetu yaweze kufanikiwa kwa faida yetu sote. Sheria hizi ni kama zifuatavyo:-

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(iii) Kushiriki kwa makini kufanya maadalio ya jioni (preparation).
(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni.
(vi) Kutunza usafi wamwili, mavazi na mazingira ya shule.
(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(ix) Kutunza mali za shule na za wengine.

**MUHIMU.**

a. **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
b. **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
c. **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule (msiba/ugonjwa).**

**04. MAKOSA YATAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kusababisha mimba.
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu.**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne (4) za wazazi/ walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi pamoja anwani na namba zao za simu.
e) Michango yote ya shule ilipwe katika akaunti namba 3261100008 (NMB BANK). Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye BANK PAY IN SLIP na kuiwasilisha shuleni. Hakuna mchango ambao si muhimu.
f) Uje na kivuli cha CHETI CHA KUMALIZA KIDATO CHA NNE (School Leaving Certificate), RESULT SLIP yako ya kidato cha nne na CHETI CHA KUZALIWA.

**NB:** Kwa siku za ivi karibuni kumekuwa na utaperi (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. ***TAFADHARI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI AU MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-***

- Mkuu wa shule : 0764017014
- Makamu Mkuu wa shule : 0679154729
- Mwandamizi Taaluma: 0688767884
- Mwandamizi malezi: 0672394584
- Matroni: 0752568950

Nakutakia kila la kheri na mafanikio tele uwapo hapa shuleni.

*N.mushi*




**NEEMA N. MUSHI**

**MKUU WA SHULE.**

FOMU NO.01

THE PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND
LOCAL GOVERNMENT AUTHORITIES.
MISSENYI DISTRICT COUNCIL
**Request for medical examination.**

Date …………………..
**PART A:**
To medical Officer
___________________________________________________________________
STUDENT'S NAME: ……………………………………………………………………………………

Please examine the above named in full as to he/ she physical and mental fitness for being able to attend to attend Secondary School. The examination should include the following categories I – IV. Each categories or sub-category of which render the applicant ineligible in case of a defect.

1. a) Eye sight ______________________________________________________
   b) Healing ______________________________________________________
   c) General physical Examination
      - Heart blood pressure.
      - Chest X-rays
   d) Speech ______________________________________________________
   e) General Disease ______________________________________________________
   f) Le prosy ______________________________________________________
   g) Urine R ______________________________________________________
   h) Stool routine ______________________________________________________

i) Sickle cell test ______________________________________________________
   j) WBC X total Differential ______________________________________________
   k) EBP include ESR ______________________________________________________
   l) Hb ______________________________________________________
 m) Khan Test on VDR ______________________________________________________

**PART B:**
I have examined the above named and consider that he/ she is physically fit/ un for being able to attend a secondary school.

DATE ……………………. SIGNATURE …………………………

DESIGNATION …………………….. HOSPITAL STAMP……………………..

**FOMU NO. 2.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI**
**SHULE YA SEKONDARI BUNAZI**

**FOMU YA KUKUBALI KUSOMA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA BUNAZI**

**SEHEMU A: MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI** (Personal Particular)
(Jaza taarifa kwa umakini, usahihi na ukweli. Hii ni siri yako na mkuu wa shule tu)

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA LA MWANAFUNZI (kama yalivyo kwenye vyeti vyako)…………………………………………………………
2. TAREHE YA KUZALIWA …………………………/…………………../……………………..
3. MAHALI ULIPOZALIWA: MKOA……………………..….WILAYA…………………………
   TARAFA…………………………KATA……………………..KIJIJI/MTAA…………………..
4. DINI……………………………DHEHEBU……………………KABILA……………………..
5. SHULE NITOKAYO………………………………………………….NAMBA YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA NNE……………………………..UFAHULU KIDATO CHA NNE: DIVISHENI……………………POINTI…………………………………
6. Jina kamili la Baba:………………………………………Kazi ya baba……………………………..
   Anwani…………………………..Namba ya simu …………………………………/…………..…………………..
7. Jina kamili la Mama…………………………………….. Kazi ya mama……………... Anwani ……………………………Namba ya simu ……………………………/…………………..

**SEHEMU B: HABARI ZINAZOWAHUSU WAZAZI/WALEZI**(Ijazwe na Mzazi/Mlezi mwenyewe)

1. Jina la baba Mzazi/Mlezi…………………………………………………… Anwani ………………………… Namba ya simu (kiganjani)…………………………… Kazi ya baba Mzazi/Mlezi………………………….. Mahali anakoishi kwa sasa: Kijiji/Mtaa……………………………………..Wilaya…………………….... Mkoa ………………………………………………………………………………………………………..
2. Jina la Mama Mzazi/Mlezi…………………………………………………Anwani………………………… Namba ya simu (kiganjani)…………………………… Kazi ya baba Mzazi/Mlezi……………………… Mahali anakoishi kwa sasa: Kijiji/Mtaa……………………………………..Wilaya…………………….... Mkoa ………………………………………………………………………………………………………..
3. Ndugu/Jamaa/ Marafiki wa karibu na muhimu wanaoweza kuwa msaada kwa mwanafunzi. Wafuatao ni ndugu/jamaa/rafiki zangu wa karibu ambao wanaweza kunisaidia kama kuna dharura . (ni vema wakawa watu wazima)

| Na. | Jina la ndugu/jamaa/rafiki | Anwani ya anapopatikana | Simu (inayopatikana) | Uhusiano |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

***Angalizo:*** Ni ndugu hao (walioandikwa hapa juu na wazazi/walezi) tu watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi hapa shuleni kwa tarehe na muda utakaopangwa na uongozi wa shule kisha wazazi/walezi kutaarifiwa.

4. Ripoti za maendeleo yake kutoka shuleni ziwe zinatumwa kwa:
   Ndugu……………………………………………….. Anwani ya posta S. L. P ………………………………..
   Simu …………………………Mahusiano yake na mwanafunzi …………………………………………..
5. Mwanafunzi ni mfuasi wa Dini/Dhehebu la ………………………………………………………………
6. Kituo cha Basi/Trani kilichopo na nyumbani ni ……………………………………………………………
7. Namba yangu ya simu kwa mawasiliano ya haraka ni ……………………………………………………
8. Mimi …………………………………………………. Bila kushinikizwa na mtu yeyote, nikiwa na akili timamu ninakubali kusoma katika shule ya sekondari Bwabuki katika Tahasusi ya ………………………na ninahaidi kusoma na kujifunza kwa bidii ili niweze kufikia malengo yangu, ya shule na ya Taifa.
   Pia ninahaidi kutojihusisha kwa aina yoyote kwenye mgomo, fujo au kosa lolote la jinai.
   Saini ya mwanafunzi……………………………………………..tarehe ……………………………………..
9. Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi)…………………………………………………… nimeridhia mwanangu asome Tahasusi aliyopangiwa ambayo ni ……………………………... katika shule ya sekondari Bwabuki. Vile vile ninahaidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu. Na ninakubaliana na sheria za shule na kanuni zake, nitalipa ada na michango ya shule kama ilivyoainishwa na kwa muda mwafaka (mapema) ili kuwezesha shughuli za shule ziweze kufanyika kama zilivyopangwa.

Saini ya Mzazi/Mlezi……………………… Tarehe ……………………..

NEEMA N. MUSHI Tarehe ……………………

MKUU WA SHULE